

nuani ya simu: "T.T.C." TUSAALE Simu Na: 0754041510 0715041510 Email:tusaalechuo@gmail.com Taifalangson2@gmail.com		Chuo cha Ualimu TUSAALE, S.L.P. 264, MAFINGA: TANZANIA: 1/07/2016
---	---	---

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Kumb.Na. TUS/TC/KUJ/03/2015

.....

**YAH: FOMU YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU NGAZI YA
 STASHAHADA KWA MWAKA 2016/2017**

1.0: UTANGULIZI:-

CHUO CHA MAFUNZO TUSAALE (TUSAALE INSTITUTE OF TRAINING)

Kimesajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) kwa namba Reg/TLF/024 (FULL REGISTRATION) na Usajili wa Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi kwa Namba CU.140.

chuo kina toa mafunzo yafuatayo:-

1. Cheti cha Maendeleo ya Jamii Ngazi ya 4
2. Cheti cha Utunzaji wa Kumbukumbu Ngazi ya 4
3. Stashahada ya Ualimu wa Elimu ya Awali na Msingi(KIINGEREZA) ngazi ya 4-6
4. Stashahada ya Ualimu wa Elimu ya Msingi(ODPE- NACTE/SERIKALI KWA KISWAHILI).ngazi 4-6

Ngazi zote hizo zipo chini ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi(NACTE)

Kulingana na mafunzo tajwa hapo juu wewe umechaguliwa na **Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (MOEVT)** kwa kupitia **Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi(NACTE)** kujiunga na **Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu wa Elimu ya Msingi (Ordinary Diploma in Primary Education-ODPE)**

Hivyo Chuo kinakupongeza kwa nafasi hii uliyochaguliwa . Tunategemea kuwa utatumia nafasi hii vizuri katika masomo yako. Hivyo unatakiwa uwe na juhudi na moyo wa kujifunza darasani na nje ya darasa ili uweze kufaulu vizuri mafunzo yako, mafunzo hayo ni ya miaka mitatu(3)

2.0: MAHALI CHUO KILIPO

Chuo kipo Mkoa wa IRINGA wilaya ya MUFINDI katika Halmashauri ya wilaya ya Mufindi mji mdogo wa nyololo, Kata ya Nyololo, kijiji cha Njiapanda Nyololo , chuo kipo Kusini Mashariki ukiwa standi ya nyololo umbali wa kilomita 1.

ILI UFIKE CHUONI TUSAALE NYOLOLO

Ukitokea Mbeya au Njombe utashukia Nyololo stand barabara kuu (Mbeya-Dar-es-salaam) unapoelekea iringa kabla ya kuufikia msitu wa taifa. Iwapo utatokea Iringa shukia nyololo ukiwa unaelea Mbeya baada ya kumaliza msitu wa taifa. Ukishuka ulizia mtu yeyote atakuonesha chuo kilipo au chukua bodaboda au tax watakufikisha chuoni.

2.1. HALI YA HEWA

Hali ya hewa ni ya baridi na nzuri sana kwa masomo. Chuo ni cha kutwa na bweni ni mchanganyiko (wanaume na wanawake) Chuo kinafundisha masomo yote ya UALIMU na MASOMO YA TAALUMA yanayofundishwa vyuo vya ualimu..

3.0: TAREHE YA KUFUNGUA:-

Chuo kitafunguliwa tarehe **09/11/2016**

masomo yanaanza mara moja baada ya chuo kufunguliwa.

3.1: MSAJILI:-

Mwanachuo ukifika Chuoni fika ofisi ya makamu mkuu wa chuo ili usajiliwe, wakati wa usajili hakikisha uwe na vitu vifuatavyo:-

- ❖ Cheti cha kuzaliwa
- ❖ Cheti halali cha kumaliza kidato cha nne
- ❖ Barua ya kuitwa chuoni
- ❖ Fomu ya kujiunga na chuo
- ❖ Vivuli vya vyeti (cha kuziliwa na kidato cha nne

KAMA HUNA VYETI WASILIANA NA MKUU WA CHUO ILI USAJILIWE .

3.4 VITU VINGINE VYA KUJA NAVYO

(hivi utakadhi kwa makamu):-

- ❖ Rimu A4 (kwa kila mwaka)
- ❖ Ndoo lita 10
- ❖ Jembe 01 lililokamilika na mpini

(Hivi utaonesha kwa matroni)

- ❖ Tranker la kuhifadhia vitu muhimu liwe na kufuli .
- ❖ Blanketi 1.
- ❖ Shuka jozi 2 za rangi ya bluu.
- ❖ Mto wenye kava ya bluu.
- ❖ Chandarua cha mbu.
- ❖ Godolo futi 2.5x6.